# Uchanganuzi wa Makosa ya Kitahajia katika Mawasiliano Andishi ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu: Mifano kutoka Chuo Kikuu cha St John's cha Tanzania

*James Omari Ontieri*[1], *Elizabeth Sakaya*[2] na *Fokas Mkilima*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Maasai Mara, Kenya*
[2]*Chuo Kikuu cha St. John's cha Tanzania, Tanzania*

**Ikisiri**

**Maandishi ya wanafunzi ni njia muhimu ya kuwasilisha hoja zao chuoni hususan katika masuala yanayohusiana na utahini. Utokeaji wa makosa katika kazi za wanafunzi ni jambo ambalo hupelekea kuvurugika kwa mawasiliano na wakati mwingine hata huwafanya wapate alama za chini wanapotahiniwa. Ingawa kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu utokeaji wa makosa katika maandishi ya wanafunzi, makosa katika maandishi ya wanafunzi wa vyuo vikuu hayajaangaziwa sana. Ni kutokana na hali hii ambapo makala haya yanalenga kutambulisha na kuainisha makosa ya kitahajia yanayojitokeza katika mawasiliano andishi ya wanafunzi wa vyuo vikuu na kupendekeza mbinu zinazoweza kutumiwa ili kupunguza utokeaji wake. Data imekusanywa kutokana na mawasiliano andishi ya wanafunzi katika mawasilisho ya semina na mijarabu ya darasani. Wanafunzi waliohusishwa kama watafitiwa ni wa mwaka wa kwanza, wa pili na wa tatu. Uchanganuzi wa data umefanywa kwa njia ya kimaelezo huku vitengo vikuu vya makosa ya kitahajia vikiwekwa wazi. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa muhimu kwa walimu wa Kiswahili kwa kuwa yatatoa mwongozo wa kuwasaidia katika kutambulisha na kuainisha makosa ya kitahajia ya wanafunzi kama njia muhimu ya kuzua mikakati ya kupunguza utokeaji wa makosa katika mawasiliano andishi ya wanafunzi wao. Aidha, wanafunzi watapata maelekezo kuhusu mbinu za kutumia ili kuboresha uandishi wao kwa kuepuka makosa anuwai yanayochanganuliwa katika makala haya. Kwa usomi wa Kiswahili, makala itachangia kuweka misingi ya uchanganuzi wa makosa anuwai yanayojitokeza katika matumizi ya Kiswahili.**

**Maneno Muhimu:** Makosa ya Tahajia, Mawasiliano, Wanafunzi, Vyuo Vikuu

## Utangulizi

Utokeaji wa makosa ya kitahajia katika kazi andishi za wanafunzi hupelekea kutingwa kwa mawasiliano lengwa. Kujitokeza kwa makosa katika kazi andishi za wanafunzi katika kiwango cha vyuo vikuu ni jambo ambalo linahitaji kushughulikiwa kwa makini kutokana na hali kwamba wahitimu hawa watakuwa na jukumu la kufundisha somo la Kiswahili katika shule za upili na hata vyuo vya ualimu. Makala haya yanachanganua makosa ya kitahajia katika vitengo vitano - udondoshaji wa sauti/silabi katika neno; uunganishaji wa kimakosa wa maneno; ubadilishaji wa fonimu; kutenganisha neno moja na kulifanya mawili kwa njia isiyo sahihi na uchopekaji wa sauti zisizohitajika katika maneno. Kama hatua ya kulishughulikia tatizo hili, tunapendekeza mbinu mbalimbali ambazo zikizingatiwa kwa makini huenda zikasaidia kupunguza makosa ambayo hujitokeza mara kwa mara katika kazi andishi za wanafunzi. Sehemu inayofuata inaonyesha makosa anuwai ya kitahajia yaliyogunduliwa na mbinu za kupunguza utokeaji wa makosa husika.

## Makosa ya Kitahajia

Tahajia ni uwakilishaji wa sauti kwa herufi katika maandishi kufuatana na mwendelezo wa maneno uliokubaliwa (TUKI, 2014). Kila lugha huwa na herufi maalumu ambazo hutumiwa kuwakilisha vitamkwa mbalimbali kwa maandishi. Uchunguzi wa fonolojia ya Kiswahili uliofanywa hadi sasa umeonyesha kwamba kuna fonimu konsonanti 25 na fonimu irabu tano (Kapinga, 1983). Ni kutokana na fonimu hizi ambapo maneno anuwai huundwa na kutumiwa katika mawasiliano. Maendelezo sahihi ni muhimu katika uundaji wa maneno yanayotumika katika lugha yoyote. Baada ya kupitia kazi andishi za wanafunzi husika, makosa yafuatayo yalijitokeza:

## Udondoshaji wa Sauti/Silabi

Ukamilifu wa neno mara nyingi huwa na umuhimu mkubwa katika mawasiliano yoyote kwa kuwa hupelekea kuwepo kwa upitishaji ujumbe kikamilifu. Katika utafiti huu, watafitiwa wengi walitumia maneno yasiyokamilika kutokana na kudondoshwa kwa sauti au hata silabi. Hali hii ilisababisha utata hususan pale ambapo neno liliathiriwa pakubwa na dosari hiyo. Mifano:

1a* … wanaamini ku^a …
2a* … na kihusishi itaku^a haina muundo mzuri…
3a* … f^lani …
4a* … sahi^i …
5a* … ndi^e …
6a* … ^izo …
7a* … m^himu …
8a* … wali^itaji …

9a* … Kilatin^ …
10a* … sitawa^i …
11a* … we^zake…
12a* … utaf^ti …
13a* … uliweza ^gundua …
14a* … ilijadiliwa na ^fasiliwa …
15a* … hi^o …
16a* … ku^eza …
17a* … ya^bwa …

Katika mfano **1a** na **2a,** sauti /w/ imedondoshwa katika maneno **kua** na **itakua** kwa mfuatano huo. Hali hii inasababisha neno jipya ambalo lina maana tofauti katika Kiswahili kutoka kwa lile mwafaka. Neno **kua** lina maana ya kuzidi kimo kadiri umri unavyoongezeka ilhali **kuwa** linamaanisha kutokea, kutendeka au kufanyika. Aidha, katika mfano **3a** na **7a,** sauti /u/ imedondoshwa katika maneno **flani** na **mhimu** na hivyo kuyafanya kuchukua muundo ambao haukubaliki katika uundaji wa maneno ya Kiswahili. Udondoshaji wa sauti /h/ katika mifano **4a, 6a, 8a na 10a** umeleta kasoro katika maneno **sahii, izo, waliitaji** na **sitawai.** Kasoro hii imejitokeza katika mazingira anuwai ambapo kuna udondoshaji uliotokea pale ambapo kuna mkururo wa irabu /i/ ambao ulistahili kuvunjwa kwa /h/ (sah**ii** na wal**ii**taji); mwingine umetokea mwanzoni mwa neno kutangulia irabu (izo) na katika silabi ya mwisho ya neno na hivyo kusababisha mkururo wa irabu (sitawa**i).** Kwa jumla /h/ inaonekana kudondoshwa pale inapotakiwa kutangulia irabu ili kuunda silabi.

Tunapochunguza mfano **5a** na **15a** tunaona kuwa sauti /y/ imedondoshwa katika mazingira yaleyale, yaani katika silabi ya mwisho ya maneno husika (ndie na hio). Hali nyingine inayojitokeza ni udondoshaji wa sauti za nazali /n/ na /m/ katika maneno **wezake** na **yabwa (11a** na **17a).** Sauti hizo za nazali zimedondoshwa katika mazingira ambapo zinatakiwa kutanguliwa na konsonanti ghuna /z/ na /b/. Hapa muungano wa sauti husika ulitarajiwa kuvyaza sauti mwambatano ‘nz’ na ‘mb’. Katika mfano **9a,** sauti /i/ imedondoshwa mwishoni mwa neno **Kilatin**. Hili ni neno ambalo limetoholewa kutokana na *Latin* na hivyo lilistahili kuwekewa sauti /i/ mwishoni ili kukubalika katika fonetiki ya Kiswahili. Katika hali nyingine watafitiwa walidondosha silabi nzima kama inavyojitokeza katika mifano **13a** na **14a** ambapo /ku/ imedondoshwa katika maneno **gundua** na **fasiliwa.** Udondoshaji huo unasababisha kasoro katika muundo wa sentensi ambamo maneno hayo yametumika. Katika mfano **16a** nusuirabu /w/ imedondoshwa na kulifanya neno **kueza** kuwa na kasoro. Maneno yaliyoendelezwa kwa njia pungufu yanaweza kusahihishwa hivi:

1b … wanaamini ku**w**a …
2b … na kihusishi itaku**w**a haina muundo mzuri…

3b … f**u**lani …
4b … sahi**h**i …
5b … ndi**y**e …
6b … **h**izo …
7b … m**u**himu …
8b … wali**h**itaji …
9b … Kilatin**i** …
10b … sitawa**h**i …
11b … we**n**zake…
12b … utaf**i**ti …
13b … uliweza **ku**gundua …
14b … ilijadiliwa na **ku**fasiliwa …
15b … hi**y**o …
16b … ku**w**eza …
17b … ya**m**bwa …

**Kuunganishwa kwa Maneno**

Maneno mbalimbali huwa na uamilifu tofauti katika sentensi. Mipaka kati ya maneno ambayo yanatumika katika sentensi kuwasilisha ujumbe ni muhimu sana na inastahili kuzingatiwa. Mipaka husika hudhihirika kwa kuacha nafasi kati ya neno moja na jingine. Kwa mujibu wa Carson (1982), uunganishaji wa maneno mawili ambayo hayana uwezekano wa kuunganishwa kirasmi, ni kosa kubwa. Endapo maneno tofauti yataunganishwa na kufanywa neno moja, ujumbe unaopitishwa utaathiriwa na huenda usieleweke kama ilivyokusudiwa. Wakieleza kuhusu muungano wa maneno Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992), wanasema kuwa hii ni mbinu ambayo kwayo maneno mawili (au zaidi) huungana na kuwa istilahi moja – inayojulikana kama istilahi ungani na inatumika sana kuundia istilahi mpya za Kiswahili. Jambo la kuzingatia ni kwamba istilahi zinazozalishwa kwa njia hii huchukuliwa kuwa neno moja na hivyo huwakilishwa kimaandishi kama neno moja bila kujali kwamba neno hilo moja limetokana na maneno mawili tofauti.

Kwa mujibu wa Temu (1984), kuna ruwaza zifuatazo za istilahi ungani: Nomino + nomino – mwana + hewa = mwanahewa; nomino + kitenzi – sitiari + ficha = sitiarifiche; nomino + kivumishi – fundi + sanifu = fundisanifu; kitenzi + nomino – pima + mvua = pimamvua; kitenzi + kitenzi – yeyusha + ungana = myeyungano. Mbali na ruwaza alizotambulisha Temu (mtaje), kuna pia muungano wa nomino + kihusishi – tabaka + nje = tabakanje. Sifa kuu ya miungano inayokubalika katika Kiswahili ni kuwa neno linalozalishwa huwasilisha dhana moja na wala siyo mbili kama inavyotokea maneno husika yanapotumika pwekepweke. Makosa yaliyogunduliwa katika kitengo hiki yalihusu uunganishaji wa vivumishi na nomino; vitenzi na nomino; viunganshi na vivumishi; viunganishi

na nomino na kadhalika. Miungano hiyo ilihusisha maneno yenye fahiwa na dhima tofauti katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno yaliyounganishwa ni pamoja na:

18a* … wasentensi ….
19a* … yakwamba ….
20a* … kwamfano ...
21a* … hivyobasi ...
22a* … kwahiyo ...
23a* … kwakutumia ...
24a* …kwakumalizia …
25a* …kwamaana …
26a* …kwasababu …
27a* …inamfumo …
28a* …unaudhaifu …
29a* …lughafulani …
30a* …anamsimamo …
31a* …hanabudi…
32a* …uliosahihi…
33a* …kwavipi …
34a* …sinahakika …

Katika mfano **18a,** mtafitiwa ameunganisha maneno mawili ambayo yalistahili kutengwa ili kuleta fahiwa iliyolengwa katika sentensi hiyo. Neno **wa** ni kivumishi cha a-unganifu ilhali **sentensi** ni nomino. Kanuni za lugha ya Kiswahili haziruhusu kuunganishwa kwa maneno hayo na hivyo kutokea kwake katika kazi andishi zilizochanganuliwa kulipelekea kuwepo kwa dosari katika tungo yalimotumika. Mfano wa **19a**, unadhihirisha kasoro inayotokana na kuunganishwa kwa vijalizo **ya** na **kwamba** ambavyo vilipaswa kutengwa na kujisimamia kama maneno kamili. Mifano **20a, 22a, 23a, 24a, 25a, 26a na 33a** (kwamfano, kwahiyo, kwakutumia, kwakumalizia, kwamaana, kwasababu na kwavipi) inaonyesha namna neno **kwa** limeunganishwa na maneno anuwai yenye uamilifu tofauti katika sentensi tofautitofauti katika kazi andishi zilizochunguzwa. Ikumbukwe kuwa katika Kiswahili neno **kwa** hutekeleza kazi mbalimbali za kisarufi na hutumiwa kama neno linalojisimamia.

Tukichukua mfano wa **26a** ambapo mtafitiwa ameandika **kwasababu,** neno **kwa** linatakiwa kutengwa na **sababu** kutokana na hali kwamba neno hilo la kwanza ni kiunganishi kinacholeta uhusiano baina ya kitendo na nia ya kutendwa kwa kitendo hicho. Kwa upande mwingine, **sababu** ni nomino inayomaanisha kitu kinachofanya kitu kingine kitokee. Hivyo basi, haya ni maneno mawili tofauti ambayo yanapaswa kutengwa mara zote yanapotumiwa katika maandishi. Katika mifano **27a, 28a, 30a, 31a na 34a,** maneno **inamfumo, unaudhaifu,**

**anamsimammo, hanabudi** na **sinahakika,** kwa mfuatano huo, yameunganishwa kwa njia inayoleta kasoro katika mawasiliano husika. Hapa watafitiwa wameunganisha vitenzi vishirikishi na nomino kuunda neno moja. Hali hii imehusisha vitenzi vishirikishi yakinishi **ina, una** na **ana (27a, 28a na 30a)** ilhali vitenzi vishirikishi kanushi **hana** na **sina** vimetumiwa katika **31a** na **34a.** Ni muhimu kuweka wazi hapa kwamba **mfumo**, **udhaifu, msimamo, budi** na **hakika** ni nomino katika lugha ya Kiswahili ambazo zinajisimamia na hivyo haziwezi kuambatishwa kwa neno lolote ili kuleta maana. Mfano **21a** unaonyesha kasoro ambapo kiunganishi **hivyobasi** kimeandikwa kama neno moja badala ya kutengwa na kuwa maneno mawili kama inavyostahili. Matumizi ya neno **lughafulani (29a),** yana upungufu kwa kuwa **lugha** ni nomino ilhali **fulani** ni kivumishi kinachotoa habari zaidi kuhusu nomino hiyo. Hivyo mtafitiwa alitakiwa kuyaendeleza kama maneno mawili tofauti. Hatimaye katika mfano **32a,** neno **uliosahihi** linastahili kutengwa na kuwa maneno mawili (ulio na sahihi) ili kukubalika kimatumizi katika Kiswahili sanifu. Hapa **ulio** ni kirejeshi ilhali **sahihi** ni kivumishi na katika hali ya kawaida huandika kama maneno mawili. Marekebisho yanaweza kufanywa kwa kuyatenga maneno yote husika hivi:

18b … wa sentensi ….
19b … ya kwamba ….
20b … kwa mfano ...
21b … hivyo basi ...
22b… kwa hiyo ...
23b … kwa kutumia ...
24b …kwa kumalizia …
25b …kwa maana …
26b …kwa sababu …
27b …ina mfumo …
28b …una udhaifu …
29b …lugha fulani …
30b …ana msimamo …
31b …hana budi …
32b …ulio sahihi…
33b …kwa vipi …
34b …sina hakika …

### Ubadilishaji wa Fonimu katika Neno

Sauti anuwai huwa na nafasi maalumu katika uundaji wa maneno katika lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili. Hali ya sauti moja kutumiwa mahali ambapo palistahili sauti tofauti, ilichangia kuwepo kwa upungufu katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa na watafitiwa. Matokeo yake yalikuwa kuandikwa kwa maneno yaliyotatiza na kutinga mawasiliano japo kwa kiwango kidogo. Ubadilishaji

mwingi uliotokea ulihusisha sauti ambazo zina sifa bainifu zenye ukuruba mkubwa hususan katika utamkaji. Aidha, ubadilishaji ulihusisha fonimu za konsonanti na zile za irabu. Maneno yaliyodhihirisha kosa la aina hii ni pamoja na:

35a* … kufiki**l**i …
36a* … se**l**ika**r**i …
37a* …mazingi**l**a
38a* … kumreje**r**ea …
39a* … taha**th**ari …
40a* … a**dh**ari …
41a* …wanafunzi waweze ku**dh**ibitisha ubantu wa Kiswahili …
42a* …lugha nyingine zilionekana hazikuwa na **dh**amani …
43a* … u**z**aifu …
44a* … waliwa**z**arau …
45a* … ili**z**oofisha …
46a* … t**i**yari …
47a* … am**p**apo …
48a* … matam**s**i …
49a* … m**u**asisi …
50a* … m**u**elekeo …
51a* … m**u**anzilishi …

Katika mifano **35a** na **37a,** fonimu /l/ imetumiwa katika nafasi ya /r/. Kosa hili limepelekea kuwepo kwa maneno ambayo hayakubaliki kimaendelezo. Mfano **36a** unadhihirisha makosa mawili ambapo /l/ na /r/ zimebadilishana nafasi kwa njia isiyokubalika katika neno **selikari.** Hali ya matumizi mabaya ya vilainisho imejitokeza katika neno **kumrejerea** ambapo /r/ ya mwisho katika neno hilo imetumika mahali palipostahili /l/. Watafitiwa husika walishindwa kung'amua tofauti kati ya sauti hizo mbili ambazo hubainishwa kwa sifa mbalimbali. Sifa kuu za kifonetiki za sauti hizi ni: Zote mbili ni vilainisho vinavyotamkwa kukiwa na mzuio mdogo tu wa mkondo-hewa; hutamkiwa kwenye ufizi; zina ughuna; /l/ inapotolewa, ulimi huwa umeinuliwa na kugusana na ufizi, hivyo, hewa hupita na kuzunguka kwenye pembe za ulimi ilhali /r/ hutolewa kwa kukunja ncha ya ulimi nyuma ya ufizi na kuuchezesha juu ya ufizi. Matumizi ya /θ/ katika mfano wa **39a**, yanaleta upungufu katika neno **tahathari**.

Ubadilishaji wa fonimu /ð/ kwa /θ/ ulitokana na ukuruba wa fonimu hizo mbili tunapochunguza sifa zao za kifonetiki. Kimsingi, /θ/ na /ð/ ni vikwamizo ambavyo hutofautishwa kwa sifa ya ughuna. Sauti /θ/ si ghuna ilhali /ð/ ni ghuna. Aidha, sauti hizi mbili hutamkiwa menoni. Fonimu hizo zimewatatiza watafitiwa zaidi tunaporejelea mifano **40a, 41a** na **42a** (adhari, kudhibitisha na dhamani) ambapo fonimu /ð/ imetumiwa katika nafasi ya /θ/ kwa njia ambayo imeleta kasoro katika maneno husika. Hapa ni wazi kuwa watafitiwa husika hawana umilisi kuhusu

matumizi ya fonimu hizi. Mifano **43a, 44a** na **45a** inaonyesha namna fonimu /z/ imetumiwa kwa njia yenye kasoro badala ya /ð/ katika maneno **uzaifu, waliwazarau** na **ilizoofisha.** Kosa hili limechangiwa na mazoea katika mazungumzo ambapo maneno husika hutumiwa katika mawasiliano bila kujali usahihi wake katika Kiswahili sanifu. Mfano **46a** unaonyesha jinsi matumizi ya irabu /i/ badala ya /a/ katika neno **tiyari** yanasababisha kasoro na kulifanya neno kutokubalika katika Kiswahili sanifu. Tatizo katika mfano **47a**, linasababishwa na matumizi ya /p/ (ampapo) mahali /b/ ilistahili kutumika. Sauti hizi mbili ziko katika kundi la vipasuo; hutamkiwa midomoni na hutofautishwa na sifa ya ughuna ambapo /b/ ni ghuna ilhali /p/ si ghuna.

Tatizo katika mfano **48a** linatokana na hali ya mtafitiwa kutumia /s/ (matamsi) badala ya /ʃ/ ambayo ndiyo sahihi. Fonimu hizi mbili ni vikwamizwa sighuna na hutamkiwa katika mazingira yenye ukuruba mkubwa. Ukuruba huo huweza kumtatiza mtafitiwa asiyekuwa makini na hivyo kusababisha matumizi yenye kasoro katika neno husika. Mifano **49a, 50a** na **51a** (muasisi, muelekeo na muanzilishi) ina kasoro kutokana na matumizi ya /u/ katika nafasi ya /w/. Watafitiwa hawakuzingatia mabadiliko ya kifonolojia ambapo vokali hubadilika na kuwa nusu vokali. Katika mazingira ambamo /u/ imetangulia vokali nyingine isipokuwa /u/ yenyewe basi irabu hiyo hubadilika na kuwa /w/ (Habwe na Karanja, 2004:63). Vokali hizi hubadilika isipokuwa pale ambapo badiliko hilo linabadilishwa na sababu za kimaana. Marekebisho yafuatayo yanaweza kufanyiwa maneno husika.

35b … kufiki**r**i …  
36b … se**r**ika**l**i …  
37b …mazingi**r**a  
38b … kumreje**l**ea …  
39b … taha**dh**ari …  
40b … a**th**ari …  
41b … ku**th**ibitisha…  
42b … lugha nyingine zilionekana hazikuwa na **th**amani  
43b … u**dh**aifu …  
44b … waliwa**dh**arau …  
45b … ili**dh**oofisha …  
46b … t**a**yari …  
47b … am**b**apo …  
48b … matam**sh**i …  
49b … m**w**asisi …  
50b … m**w**elekeo …  
51b … m**w**anzilishi …

**Kutenganisha Neno**

Maneno kamili ni muhimu katika uwasilishaji ujumbe katika lugha yoyote ile. Wakati ambapo neno moja hutengwa na kufanywa mawili na zaidi, mawasiliano huathiriwa japo kwa kiasi kidogo. Kasoro hii ya kutenganisha maneno hutokea mara nyingi katika maandishi kutokana na ukosefu wa umilisi kuhusu maumbo ya maneno yanayokubalika katika lugha. Katika insha tulizozichunguza, maneno yaliyotengwa zaidi ni vitenzi vilivyosheheni 'o' rejeshi. Aidha, maneno ya uradidi nayo yalitengwa ingawa kwa kiwango kidogo. Maneno yaliyotengwa ni pamoja na:

52a* … iliyo chaguliwa…
53a* … ulio ainisha …
54a* … inayo agiza …
55a* … kinacho msaidia
56a* … zinazo mwongoza…
57a* … zitakazo kuelekeza …
58a* … zinazo leta …
59a* … kinacho kusudiwa…
60a* … tofauti tofauti...
61a* … mmoja mmoja …
62a* … mbali mbali …
63a* … vile vile …
64a* … mwana zuoni …
65a* … wana mapokeo …
66a* … wana sarufi…
67a* … hali kadhalika …
68a* … zili kuwa …

Maneno yanayotokea katika mifano kati ya nambari **52a** hadi **59a**, ni vitenzi ambamo 'o' rejeshi imetumika. Kutengwa kwao kunatokea pale ambapo 'o' rejeshi imeishia na hivyo sehemu ya kwanza ya neno kuchukuliwa kama neno kamili na vilevile ile ya pili. Kosa hili limesababishwa na ukosefu wa umilisi katika matumizi ya 'o' rejeshi inapochopekwa ndani ya kitenzi na pale inapoambishwa kwenye 'amba'. Tofauti kati ya 'o' rejeshi katika mazingira hayo mawili ni kuwa inapotumiwa katika kitenzi, neno hilo halitengwi ilhali inapoambishwa kwenye 'amba', tunapata maneno mawili. Kwa mfano tukitumia 'amba' katika mfano wa **52a**, tutapata maneno mawili – **ambayo ilichaguliwa.** Mabadiliko haya yalitatiza watafitiwa na hivyo kupelekea kutengwa kwa vitenzi ambamo 'o' rejeshi ilitumiwa. Mifano **60a** hadi **63a**, inaonyesha namna maneno ya uradidi yalivyotengwa kimakosa. Kimsingi, haya ni maneno ambayo hutumiwa kusisitiza jambo au kitendo kinachozungumziwa kwa kurudia neno zima au sehemu ya neno. Ili kuleta maana inayonuiwa, maneno ya uradidi hustahili kutokea kama neno moja. Aidha, katika maneno ya aina hii, mkazo huwekwa kwenye silabi moja na wala

siyo mbili. Nayo mifano **64a**, **65a, 66a** na **67a**, inadhihirisha kutengwa kimakosa kwa maneno mwambatano ambayo kimsingi yanatakiwa kuandikwa kama neno moja kwa kuwa huwakilisha dhana moja. Hali hii ilitokana na ukosefu wa umilisi kuhusu uundaji na matumizi ya maneno mwambatano katika lugha ya Kiswahili. Katika mfano **68a,** neno husika limetengwa na kuwa mawili kwa njia isiyokubalika. Ikumbukwe kwamba sehemu ya kwanza inasheheni viambishi pekee na hivyo kwa vyovyote vile haiwezi kutengwa na kufanywa neno kamili.

Kwa jumla makosa mengi yaliyotokea katika kitengo hiki yanaashiria kwamba watafitiwa hawakujua neno halisi na lililokubalika katika Kiswahili sanifu hali iliyopelekea neno moja kutengwa na kufanywa mawili. Hapa watafitiwa husika walishindwa kufikiria kwa kina ikiwa hayo maneno baada ya kutengwa yalikuwa na maana yoyote. Aidha, kutokana na maneno husika kuonekana kuwa marefu, watafitiwa walichukulia kuwa yalistahili kukatwa na kufanywa mawili. Ni muhimu ikumbukwe kuwa Kiswahili ni lugha yenye muundo gubi ambapo viambishi hutumika katika kuongezea usarufi wa maneno. Katika Kiswahili maneno huunganishwa ili kuukamilisha usarufi. Hivyo basi, kutengwa kwa neno moja na kufanywa mawili kusingetokea katika kazi andishi za watafitiwa ikiwa wahusika wangekuwa na umilisi kuhusu umuundo gubi wa lugha ya Kiswahili. Mifano hiyo inaweza kurekebishwa hivi:

52b … iliyochaguliwa…
53b … ulioainisha …
54b … inayoagiza …
55b … kinachomsaidia
56b … zinazomwongoza…
57b … zitakazokuelekeza …
58b … zinazoleta …
59b … kinachokusudiwa…
60b … tofautitofauti...
61b … mmojammoja …
62b … mbalimbali …
63b … vilevile …
64b … mwanazuoni …
65b … wanamapokeo …
66b … wanasarufi…
67b … halikadhalika …
68b … zilikuwa …

### Uchopekaji wa Sauti/Silabi Isiyohitajika

Maneno kamili yanapoongezwa sauti au silabi isiyohitajika, matokeo ni kuvurugika kwa maumbo ya maneno husika na utata katika uwasilishaji wa ujumbe. Katika kazi andishi tulizozichanganua, uchopekaji wa sauti ulihusisha fonimu za

konsonanti na zile za irabu. Tatizo la uchopekaji wa irabu hususani /u/ na /i/ limechangiwa pakubwa na muundo wa Kibantu ambao ni wa silabi wazi. Muundo huu ndio ulioingizwa katika Kiswahili kwa njia isiyokubalika kutokana na ukiushi wa Kiswahili baada ya kupitia mabadiliko mbalimbali. Sauti ambazo zilichopekwa katika maneno mengi yaliyokuwa na dosari ni: /u/, /i/, /h/ na /n/. Makosa katika kipengele hiki yanadhihirika katika mifano ifuatayo:

69a* … tath**i**mini …
70a* …watu wanapaswa kupima ar**i**dhi ili wapate hati ya kumiliki …
71a* … uta**a**ratibu …
72a* …muk**u**tadha …
73a* … m**u**milisi …
74a* … m**u**husika …
75a* … inam**u**husu …
76a* … maneno yenye **u**thamani …
77a* … **u**wingi …
78a* … **h**ulianzishwa …
79a* … **h**ulikuwepo …
80a* … ki**h**isimu …
81a* … ilichuku**w**a …
82a* … mta**n**zamo …
83a* … walie**n**gemea sana kuchambua …
84a* … kawai**n**da…
85a* … amba**n**zo …

Mifano **69a** na **70a** (tathimini na aridhi) inadhihirisha namna uchopekaji wa /i/ umefanywa na hivyo kusababisha kasoro katika maendelezo ya maneno husika. Kimsingi maneno hayo yana asili ya Kiarabu na huendelezwa bila hiyo /i/ iliyochopekwa. Uchopekaji huu umetokana na imani kwamba maneno yote mkopo yanapoingizwa katika Kiswahili huendelezwa kwa kutumia mfumo uliozoeleka katika lugha za Kibantu ambapo silabi huundwa kwa konsonanti na irabu (KI). Hali sawa na hii imejitokeza katika mifano **71a, 72a, 73a, 74a** na **75a** (utaaratibu, mukutadha, mumilisi, muhusika na inamuhusu), ambapo /a/ imechopekwa katika neno la kwanza na /u/ katika maneno manne yanayofuata kwa njia isiyokubalika katika Kiswahili sanifu.

Uchopekaji wa /a/ umetokana na mtafitiwa kukosa makini katika uendelezaji wa neno husika. Kwa upande mwingine uchopekaji wa /u/ umechukua mfumo wa uchopekaji wa /i/ katika mifano 69a na 70a hapo juu. Katika mifano **76a** na **77a** (uthamani na uwingi), mtafitiwa amechopeka /u/ mwanzoni mwa nomino husika kwa njia yenye kasoro. Nomino husika huwa kamilifu bila hiyo /u/ iliyochopekwa. Mifano **78a, 79a na 80a** (hulianzishwa, hulikuwepo na kihisimu) inadhihirisha uchopekaji wa /h/ kwa njia inayoyafanya maneno husika kuwa na kasoro. Hali hii

imetokana na mazoea katika matamshi ambapo watumiaji wengine wa lugha ya Kiswahili huongeza sauti /h/ kabla ya irabu katika maneno anuwai katika matamshi. Mazoea haya ndiyo yamepenyezwa katika maandishi na matokeo yake ni maneno yasiyokubalika kimaendelezo katika Kiswahili sanifu. Katika mfano **81a**, sauti /w/ ilichopekwa katika silabi ya mwisho ya kitenzi husika na kukifanya pungufu. Katika Kiswahili, maendelezo ya aina hiyo hukubalika katika ushairi hususani kutokana na uhuru wa kishairi. Mtafitiwa husika hajaweka mipaka kati ya lugha ya kishairi na ile rasmi ambayo hutumika katika maandishi nathari ya Kiswahili. Aidha, kasoro hii imetokana na athari ya kilahaja ambapo mwanafunzi aliliendeleza neno husika kama linavyoendelezwa katika lahaja ya Kiamu. Nayo mifano **82a, 83a, 84a** na **85a** (mtanzamo, waliengemea, kawainda na ambanzo) inaonyesha uchopekaji wa /d/. Hapa uchopekaji umetokea katika mazingira yenye uwiano ambapo /d/ imeongezwa kabla ya konsonanti ghuna /z, g na d/. Matokeo ya uchopekaji huo ni maneno ambayo hayakubaliki katika Kiswahili sanifu. Maendelezo sahihi ya maneno hayo ni:

69b … tathmini …
70b …watu wanapaswa kupima **ardhi** ili wapate hati ya kumiliki …
71b … utaratibu …
72b …muktadha …
73b… mmilisi …
74b … mhusika …
75b … inamhusu …
76b … maneno yenye **thamani** …
77b … wingi …
78b … ulianzishwa …
79b … ulikuwepo …
80b … kiisimu …
81b … ilichukua …
82b … mtazamo …
83b … waliegemea sana kuchambua …
84b … kawaida…
85b … ambazo …

**Mbinu za Kupunguza Utokeaji wa Makosa ya Kitahajia**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, watafitiwa mbalimbali wanadhihirisha udhaifu wa kipekee kuhusiana na tahajia. Kunazo aina tofauti za makosa ya kitahajia. Mwanafunzi anapaswa kuandika orodha ya maneno ambayo humkanganya anapowasilisha mawazo yake kimaandishi. Hapa mwanafunzi ajikite katika kutambua makosa telezi ambayo huwa rahisi kutokea katika uandishi. Haya ni makosa yanayohusisha sauti tatizi kama vile /r/ na /l/, /b/ na /p/, /f/ na /v/, /s/ na /z/ miongoni mwa nyingine. Kupitia kwa utambuzi wa makosa telezi, mwanafunzi

mara nyingi atakuwa na tahadhari kubwa wakati wa uandishi wake ili kuyaepuka. Katika juhudi za kuyatambua makosa ya aina hiyo mwanafunzi anashauriwa:

i) Kusoma vitabu mbalimbali vinavyotoa maelezo kuhusu uandishi bora hasa katika kipengele cha tahajia.
ii) Kujifunza matumizi sahihi ya sauti katika matamshi ya lugha husika.
iii) Kujifunza sauti katika lugha husika kwa kusoma vitabu vya fonolojia na kujifunza kutoka kwa wazawa wa lugha hiyo.
iv) Kusoma vitabu vinavyozungumzia makosa ya kitahajia.

Aidha, mwanafunzi anashauriwa atayarishe chati ya tahajia ambayo itamsaidia kufuatilia kwa makini maneno au maumbo mengine ambayo humtatiza. Kielelezo kinachofuata kinaweza kutumiwa:

**Kielelezo: Chati ya Tahajia**

| **Tahajia yangu** | **Tahajia lengwa** | **Herufi tatizi n.k** |
|---|---|---|
| Kua | Kuwa | a/wa |
| Hanabudi | Hana budi | Neno moja = maneno mawili |
| Zitakazo kuelekeza | Zitakazokuelekeza | Maneno mawili = neno moja |
| Flani | Fulani | f/fu |
| Kufikili | Kufikiri | l/r |
| Matamsi | Matamshi | s/sh |
| Tahathari | Tahadhari | th/dh |
| Uzaifu | Udhaifu | z/dh |
| Muhusika | Mhusika | mu/m |

Asili: Kimetoholewa kutoka kwa Ontieri, 2010

Kufuatilia maneno tatizi ni hatua muhimu katika kuimarika kwa kiwango cha mwanafunzi katika tahajia (Pickett na Laster, 1972; Hubbard, 1988). Mwanafunzi akitambua aina ya makosa inayomkwaza anapoandika, itakuwa rahisi kurekebisha makosa ya uendelezaji wa maneno husika na hata katika mengine yanayochukua ruwaza kama hiyo (Newby, 1989). Kwa mujibu wa Newby (mtaje), mwanafunzi anastahili kufikiria jinsi neno linavyoendelezwa kwa misingi ya muundo wake. Neno huwa na sehemu mbalimbali – za irabu na konsonanti. Kila neno lina mwanzo, kati na mwisho. Iwapo mwanafunzi atajifunza kutambua namna herufi hupangwa ili kuunda neno, basi atakuwa katika nafasi nzuri ya kuendeleza maneno kisahihi.

Katika juhudi za kuboresha umilisi wa kitahajia, inambidi mhusika asome vitabu vingi iwezekanavyo. Hapa msisitizo uwekwe kwenye usomaji wa vitabu vinavyolekeza kuhusu matumizi ya sauti katika lugha – fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Aidha, kamusi iwe kitabu cha kimsingi kwa kila mwanafunzi wa somo la Kiswahili kama njia ya kusisitiza maendelezo sahihi ya maneno. Mwanafunzi akiwa na shaka na tahajia ya neno lolote basi ashauriwe alitafute katika kamusi ili

kuwa na uhakika wa maendelezo sahihi (Pickett na Laster, 1972; Newby, 1989; Greenberg, 1988). Unapoangalia maumbo ya maneno mara kwa mara, maumbo hayo hukuganda akilini. Baadhi ya aina za makosa ya kitahajia zinazojitokeza mara kwa mara hutokana na:

i) Maneno yanayokaribiana kimatamshi na kimaendelezo kama vile **kua** na **kuwa**
ii) Maneno yaliyounganishwa kimakosa kama vile **kwasababu**, **kwahiyo**….
iii) Maneno yaliyotengwa kimakosa kama vile **zinazo leta**, **mbali mbali** ….
iv) Udondoshaji wa sauti/ silabi kama vile **ndi^e, f^lani**….
v) Ubadilishaji sauti katika neno kama vile taha**th**ari, u**z**aifu ….
vi) Uchopekaji wa sauti/silabi kama vile **h**ulianzishwa, ki**h**isimu….

Stadi ya kuandika inastahili itiliwe mkazo katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hali hii itapelekea wanafunzi kufikia kiwango cha juu cha umilisi wa maumbo sahihi katika uandishi. Ikumbukwe kwamba wanafunzi huwasilisha kazi zao kwa maandishi kuliko stadi nyingine hasa tunapochunguza suala la utahini. Hivyo, wanafunzi waelekezwe vyema kuhusu silabi, viambishi na maneno. Wapewe mazoezi ya kuandika huku wakisisitiziwa juu ya sheria za kiuandishi na umuhimu wao katika kuvyaza tungo zinazokubalika katika Kiswahili sanifu. Pia, wanapofundisha stadi ya kuandika, walimu wasiyapuuze makosa yanayojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wao. Wayachukue makosa hayo kama msingi wa kuwaelekeza wanafunzi hao kuhusu njia za kuyaepuka makosa husika na hivyo kuboresha uandishi wao. Ikiwezekana kutengwe wakati maalumu wa kushughulikia makosa ya kitahajia yanayotokea mara kwa mara katika uandishi wa wanafunzi. Hatua hii itakuwa njia muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kuelewa mbinu za kutumia katika kurekebisha makosa yanayojitokeza katika uandishi wao.

Mbinu nyingine zinazoweza kutumiwa na mwanafunzi katika juhudi za kupunguza utokeaji wa makosa ya kitahajia ni pamoja na:

i) Kutamka maneno anayonuia kuandika ile awe na uhakika kuhusu vitamkwa vinavyounda neno husika (Pickett na Laster, 1972; Carson, 1982).
ii) Kudurusu kile ambacho ameandika kwa kuwa makosa mengine ya kitahajia ni wazi na huweza kurekebishwa kwa urahisi.
iii) Kuandika neno analoliendeleza vibaya mara kwa mara huku akilihusisha na taswira fulani ili limgande akilini.
iv) Kujaliza fumbo ambalo aghalabu humhitaji kuonyesha uhusiano kati ya neno na tahajia (Greenberg, 1988).

## Hitimisho

Makala haya imeshughulikia makosa ya kitahajia ambayo yamejitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa vyuo vikuu wanaojikita katika Kiswahili. Tumeyagawa makosa tuliyoyagundua katika vitengo vitano. Kwanza, kuna makosa ya udondoshaji wa sauti/ silabi ambapo maneno mengi yaliyodhihirisha kasoro hii yalikosa sauti ama ya irabu au konsonanti na kupelekea maneno husika kutokubalika katika Kiswahili sanifu. Pili, uunganishaji wa kimakosa wa maneno mawili na kuyafanya kuwa moja hususani vivumishi na nomino, viunganishi na nomino, vitenzi na nomino na viunganishi na vivumishi. Tatu, ubadilishaji wa fonimu katika maneno ambapo sauti tatizi zilidhihirisha matumizi yenye kasoro ni pamoja na /r/ na /l/, /θ/ na /ð/ na /z/ na/ð/. Nne, kutenganisha neno moja na kulifanya mawili kwa njia isiyo sahihi hasa katika maneno yaliyotumia 'o' rejeshi, maneno mwambatano na yale ya uradidi. Tano, uchopekaji wa sauti zisizohitajika katika maneno ambapo sauti zilizochopekwa katika maneno mengi ni /u/, /i/, /h/ na /n/. Hatimaye, makala imeweka wazi mbinu za kupunguza utokeaji wa makosa ya kitahajia katika kazi andishi za wanafunzi. Mbinu zilizopendekezwa ni pamoja na: Mwanafunzi kuwa na orodha ya maneno tatizi; chati ya maumbo tatizi; usomaji wa vitabu anuwai na kusisitizwa kwa stadi ya kuandika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

**Marejeleo**

Carson, B. R. (1982). *A Basis for Composition*. Columbus, Ohio: Bell & Howell Company.

Greenberg, K. L. (1988). *Effective Writing: Choices and Conventions*. New York: St. Martin's Press Inc.

Hubbard, P. (1988). Language Teaching Approaches, the Evaluation of CALL Software, and Design Implications. In W. Flint (Mh.), *Modern Media in Foreign Language Education: Theory & Implementation, 227 -254.* Lincolnwood, IL: National Textbook Company. Retrieved February 12, 2010 from https://www.calico.org/p-172-Zebras%204.4%20(82003).html

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Newby, M. (1989). *Writing: A Guide for Students.* Cambridge: Cambridge University Press.

Ontieri, J. O (2010). *Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Pickett, A. N. na Laster, A. (1972). *Handbook for Student Writing.* New York: Harper & Row Publishers, Inc.

Temu, C. W. (1984). Kiswahili Terminology: Principles Adopted for the Enrichment of the Kiswahili Language. *Kiswahili Juz. 51/1 & 51/2: 112 – 126.*

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Tumbo-Masabo, Z. N. Z. na Mwansoko, H. J. M. (1992). *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.